Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania: Muhtasari

Imetayarishwa na UNICEF kutoka kwenye Ripoti ya *"Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania. Matokeo ya Utafiti wa Kitaifa, 2009: Muhtasari wa Kuenea kwa Ukatili wa Kijinsia, Kimwili na Kiakili, Muktadha wa matukio ya Ukatili wa Kijinsia, Afya na Athari ya Tabia ya Ukatili iliyotokea utotoni, Dar es Salaam, Tanzania",* UNICEF Tanzania, Kitengo cha Kuzuia Ukatili, Kituo cha Kitaifa cha kuzuia na Kudhibiti Ukatili, Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa, Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya ya Sayansi na Tiba cha Muhimbili, 2011.

Jamhuri ya Muungano Tanzania
Agosti 2011

unicef
unite for children

© Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto

Picha ya Jalada: UNICEF/Julie Pudlowski

Ruhusa ya kudurufisha sehemu yoyote ya andiko hili ni kwa kibali tu.
Tafadhali wasiliana na:

Idara ya Mawasiliano, Utetezi na Ushirikiano
UNICEF Tanzania
P.O Box 4076
Dar es Salaam
Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Simu: +255 22 219 6600
Barua pepe: daressalaam@unicef.org

Kibali kitatolewa bure kwa matumizi ya elimu na mashirika ya jamii..
Wengineo wanaweza kuombwa kulipia ada ndogo

Dar es Salaam, Mei 2011

IBSN: 9987-443-05-2

Yaliyomo

1. Utangulizi **7**

2. Kuenea kwa ukatili wa kijinsia, kimwili na kiakili kwa watoto Tanzania **9**

Ukatili wa kijinsia utotoni
Ukatili wa kimwili utotoni
Ukatili wa kiakili utotoni
Muingiliano wa aina za ukatili utotoni

3. Ukatili Dhidi ya Watoto: ni nani, wapi na wakati gani? **15**

Ni nani wanaofanya ukatili wa kijinsia?
Ni nani wanaotenda ukatili wa kimwili?
Ni nani wanaofanya ukatili wa kiakili?
Watoto huwa hatarini zaidi wapi na wakati gani?

4. Athari za ukatili dhidi ya watoto: kwa nini ni muhimu **23**

Ukatili utotoni na uwezo wa kutafuta msaada
Ukatili utotoni na afya za Watanzania
Ukatili utotoni na tabia hatarishi
Ukatili utotoni na Upimaji wa VVU

5. Mitazamo kuhusu ukatili na unyanyaswaji Tanzania **29**

Unyanyasaji mke/mume
Unyanyaswaji wa watoto kijinsia
Ukeketaji/tohara ya wanawake

6. Tanzania itafanya nini kukabili tatizo la ukatili dhidi ya watoto? **33**

Kiambatisho: Methodolojia ya Utafiti wa Ukatili wa Watoto Tanzania 2009

Akronimi

Fasili na istilahi muhimu

Wachangiaji

Michoro

Mchoro 1: Ukatili wa kijinsia, kimwili na kiakili uliotokea utotoni. Taarifa za wenye umri wa miaka 13 hadi 24

Mchoro 2: Asilimia ya wenye miaka 13 hadi 17 waliotendewa ukatili wa kijinsia mara nyingi. Taarifa za wenye umri wa miaka 13 hadi 17 waliotendewa ukatili wa kijinsia.

Mchoro 3: Aina ya ukatili uliotokea utotoni kabla ya kutimiza umri wa miaka 18. Taarifa za wenye umri kati ya miaka 13 na 24.

Mchoro 4: Umri wakati tukio la kwanza la ukatili wa kijinsia lilitokea. Taarifa za wenye umri wa miaka 18-24 waliokumbwa na ukatili wa kijinsia utotoni.

Mchoro 5: Aina ya ukatili wa kimwili. Taarifa za wenye miaka 13 hadi 24 waliokumbwa na ukatili wa kimwili utotoni.

Mchoro 6: Aina za ukatili wa kiakili utotoni. Taarifa za wenye miaka 13 hadi 24 (Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania 2009)

Mchoro 7: Waathirika wa ukatili wa kijinsia utotoni ambao pia walikumbwa na ukatili wa kimwili na kiakili utotoni. Taarifa za walio na miaka 13 hadi 24.

Mchoro 8: Tofauti ya umri kati ya mkosaji wa ukatili wa kijinsia na waathirika wa kike. Taarifa za waathirika wa ukatili ya kijinsia wenye miaka 13 hadi 24.

Mchoro 9: Aina ya nguvu au ushurutishaji uliotumika katika tukio au jaribio la kwanza la ngono ya kulazimishwa utotoni. Taarifa za wenye miaka 13 hadi 24.

Mchoro 10: Watendaji wa ukatilii wa kimwili kwa watoto- taarifa za wenye miaka 13 hadi 24.

Mchoro 11: Idadi ya matukio ya ukatili dhidi ya wenye umri kati ya 13 hadi 17 ya kupigwa ngumi, kupigwa teke na kuchapwa na ndugu.

Mchoro 12: Idadi ya matukio ya wenye umri wa miaka 13 hadi 17 waliotoa taarifa za kupigwa ngumi, kupigwa teke na kuchapwa na mwalimu.

Mchoro 13: Waliotenda ukatili wa kiakili kwa watoto. Taarifa za waathirika wa ukatili ya kiakili wenye miaka 13 hadi 24.

Mchoro 14: Muda katika siku ambapo tukio la kwanza la ukatili wa kijinsia lilifanyika dhidi ya wasichana kama ilivyoarifiwa na wenye miaka 13 hadi 24.

Mchoro 15: Sababu za kutomwambia mtu yoyote tukio la ukatili wa kijinsia lililotokea utotoni. Taarifa za waathirika wa ukatili ya kijinsia wenye miaka 13 hadi 14 ambao hawakumweleza mtu.

Mchoro 16: Waathirika wa ukatili wa kijinsia waliomwambia mtu, walioomba na kupata huduma. Taarifa za wavulana na wasichana wenye miaka 13 hadi 24.

Mchoro 17: Wasiotumia au waliotumia kondomu kwa nadra katika miezi 12 iliyopita ambao waliwahi kutendewa ukatili wa kijinsia utotoni. Taarifa za vijana wenye miaka 19 hadi 24 waliowahi kujamiiana.

Mchoro 18: Washirika wengi wa ngono katika miezi 12 iliyopita wa waathirika wa ukatili wa kijinsia utotoni. Taarifa za wenye miaka 19 hadi 24 waliowahi kujamiiana.

Mchoro 19: Wanaounga mkono mume kumpiga mkewe kwa sababu moja au zaidi, kwa wale waliowahi kutendewa ukatili wa kimwili na ndugu utotoni. Taarifa za wenye miaka 13 hadi 24.

Jedwali

Jedwali 1: Waliotenda ukatili wa kijinsia. Taarifa za wenye miaka 13 hadi 24.

Jedwali 2: Kuenea kwa ukatili wa kimwili unaotekelezwa na ndugu. Taarifa za wenye miaka 13 hadi 24.

Jedwali 3: Kuenea kwa ukatili wa kimwili unaotekelezwa na waalimu wa kike na kiume kwa taarifa za wenye miaka 13 hadi 24.

Jedwali 4: Maeneo ya matukio ya ukatili wa kijinsia kwa wenye umri 13 hadi 24.

Istilahi na fasili muhimu

Mtoto: mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka 18, hivyo ukatili wa utotoni maana yake ni ukatili wa aina yoyote ambao ulitokea kabla ya mtoa taarifa hajatimiza umri wa miaka 18.

Unyanyaswaji kijinsia utotoni: Watoto wanaopokea pesa au vitu ili wafanye ngono: yoyote mwenye umri wa chini ya miaka 18 anaepokea pesa au vitu kwa kufanya ngono.

Ukatili wa Kiakili: Ukatili wa kiakili kama vile kuitwa majina mabaya, kuonyeshwa kwamba hutakiwi, au kutishiwa kuachwa au kutelekezwa

Tohara ya wanawake/Ukeketaji: aina zote zinazotumika kukata au kukeketa sehemu ya uke yote, au kidogo, ya au kujeruhi kwa njia nyingine sehemu za uke kwa sababu ambazo si za kitabibu au kiafya.

Yatima: mtu yoyote aliye chini ya umri wa miaka 18 aliyefiwa na mzazi mmoja au wote wawili

Ukatili wa kimwili: vitendo vya ukatili wa kimwili kama kupigwa kofi, kusukumwa, kupigwa ngumi, kuchapwa au kutishiwa na silaha kama bunduki au kisu.

Kujamiiana (kwa maana ya kufanya ngono kwa mara ya kwanza): Kujamiiana maana yake pale ambapo uume wa mwanaume unapoingia kwenye uke au mkundu wa mwingine, hata kama unaingia kidogo tu.

> **Kujamiiana kwa wanawake (inapotumika kwa ukatili wa kijinsia):** ni pamoja na mtu kumuingilia mwanamke kwenye uke au mkundu na uume wake, mikono yake, vidole vyake, mdomo wake au kitu chochote au kumuingilia mdomoni na uume wake.
>
> **Kujamiiana kwa wanaume (inapotumika kwa ukatili wa kijinsia):** ni pamoja na mtu kumuingilia mwanaume mkunduni na uume wake, mikono yake, mdomo wake, au vitu vingine au kuingiza uume wa mtu mwingine mdomoni mwake; hii inaweza kuwa pamoja na kuingiza uume wa mwanaume bila ridhaa yake kwenye mdomo, uke au mkundu wa mwingine.

Ukatili wa Kijinsia: Ukatili wa kijinsia ni tendo analotendewa mtu mwingine bila ridhaa yake ambalo linajumuisha makosa ya kujamiiana bila ridhaa (kubaka), jaribio la kujamiiana bila ridhaa, kumgusa kijinsia pasipo ridhaa au kutomasa (kumgusa mtu sehemu asizotaka), na unyanyasaji bila kugusana (k.m. vitisho vya kutumia nguvu kijinsia, ujitwazaji kingono, kubugudhi kwa maneno ya kijinsia).

Jaribio la kujamiiana bila ridhaa: Pale ambapo mkosaji anajaribu kujamiiana na mtu asiyeridhia, lakini bila mkosaji kufanikiwa.

Kujamiiana kwa kulazimishwa: Mkosaji anapomshinikiza au kumlazimisha mwenzi wa kike au kiume kufanya ngono kinyume cha matakwa yake. Kwa mfano, mwenzi anapojamiiana bila kutaka kwa sababu ya mabishano na kushinikizwa.

Kujamiiana kwa nguvu: Mkosaji anapotumia nguvu za kimwili kumlazimisha mwenzi wake kufanya ngono.

Mwenzi kuguswa bila ridhaa yake: Mkosaji anapomgusa mwingine bila ridhaa yake kijinsia, kwa mfano anapomgusa bila anaeguswa kutaka, kubusu bila ridhaa, kukamata au kutomasa bila ridhaa lakini bila kujaribu kumlazimisha kufanya ngono.

Akronimi

WMJJW Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto
KKKSM Kikosi Kazi Kinachojumuisha Sekta Mbalimbali
UUDWT Utafiti wa Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania

Muhtasari wa Matokeo

Ukatili wa Kijinsia

- Karibu wasichana 3 kati ya 10 na mvulana 1 kati ya 7 wameripoti kutendewa walau tukio moja la ukatili wa kijinsia kabla ya kutimiza umri wa miaka 18.
- Karibu asilimia 6 ya wasichana wamelazimishwa kujamiiana kabla hawajatimiza miaka 18. Marafiki, majirani, na watu wasiowafahamu walitajwa na wasichana na wavulana kama wakosaji wa ukatili wa kijinsia.
- Wakosaji walio wengi wa ukatili wa kijinsia dhidi ya wasichana walikuwa wana umri mkubwa kuliko waathirika, na wakosaji walio wengi dhidi ya wavulana walikuwa takribani umri mmoja na waathirika.
- Matukio ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wasichana na wavulana yalitokea mara nyingi zaidi nyumbani kwa mtu, shuleni au njiani kwenda au kutoka shule.
- Matukio yaliyo mengi ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wasichana na wavulana yalitokea kati ya adhuhuri na saa 2 usiku.

Ukatili wa Kimwili

- Takribani robo tatu ya wasichana na wavulana wameripoti kufanyiwa ukatili wa kimwili kabla ya kutimiza miaka 18.
- Takriban wasichana 6 kati ya 10 na wavulana wameripoti kufanyiwa ukatili wa kimwili na ndugu na 1 kati ya 2 na waalimu.

Utafutaji Msaada na Huduma zilizopatikana kwa Waathirika wa Ukatili wa Kijinsia wenye Umri wa miaka 13 hadi 24

- Takriban nusu ya wasichana na theluthi ya wavulana ambao walifanyiwa ukatili wa kijinsia kabla ya kutimiza miaka 18 walimwambia mtu.
- Takriban msichana 1 kati ya 5 na mvulana 1 kati ya 10 walitafuta huduma baada ya kufanyiwa ukatili wa kijinsia kabla ya kutimiza miaka 18.
- Takriban msichana 1 kati ya 8 na mvulana 1 kati ya 20 alipata huduma kufuatia tukio la ukatili wa kijinsia lilomsibu kabla ya kutimiza miaka 18.

Matendo ya Ukatili utotoni na Afya ilivyo sasa

- Wasichana walioripoti kufanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia, kimwili na kiakili utotoni waliripoti hali mbaya zaidi ya afya kiakili na hata kimwili kuliko wasichana wengine.
- Wavulana walioripoti kufanyiwa ukatili wa kiakili utotoni, waliripoti afya mbaya zaidi kiakili na kimwili kuliko wavulana wengine. Lakini, afya ya kiakili na kimwili ya wavulana walioripoti kufanyiwa ukatili wa kijinsia ilifanana na ya wavulana wengine.

Ukatili wa Kijinsia na VVU/UKIMWI

- Waathirika wa Ukatili wa Kijinsia utotoni na ufahamu wa sehemu za kupima UKIMWI na ufahamu wa kupimwa UKIMWI havikuonyesha uhusiano wowote kitakwimu kwa wasichana na wavulana.
- Mazoea ya kuwa na washirika 2 au zaidi wa ngono katika miezi 12 iliyopita yalikuwa juu zaidi miongoni mwa wasichana na wavulana wa miaka 19 hadi 24 wenye historia ya kufanyiwa ukatili wa kijinsia utotoni.

Matokeo Mengineyo

- Takriban asilimia 60 ya wasichana na zaidi ya asilimia 50 ya wavulana wenye miaka 13 hadi 24 wanaamini ni sawa kwa mume kumpiga mkewe katika mazingira fulani maalum au kwa sababu fulani maalum.
- Asilimia 5.2 ya wasichana wenye miaka 13 hadi 17 waliripoti kufanyiwa tohara na asilimia 9.6 ya wasichana wenye miaka 18 to 24 waliripoti kutahiriwa.

Picha: UNICEF/Hiroki Gomi

1. Utangulizi

Vitendo vya ukatili dhidi ya watoto ni suala zito la haki za binadamu, jamii na afya ya jamii nchini Tanzania kama ilivyo katika nchi nyingi duniani. Vitendo hivi vinamomonyoa msingi imara ambao watoto wanahitaji ili wawe na afya bora na maisha yenye tija, na vinasigana na haki ya msingi ya watoto ya kuishi salama utotoni. Tatizo la ukatili wa kijinsia, ambalo ndilo hasa linalozungumziwa na Utafiti wa 2009 juu ya Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania ni zito sana.[a] Kuainisha aina zote za vitendo vya ukatili (kijinsia, kimwili na kiakili) na sababu zake ni hatua muhimu kuelekea kwenye kubuni mikakati na sera za kitaifa zinazohusisha sekta mbalimbali, za kuzuia na kukabiliana na tatizo hili na kuwalinda vizuri zaidi watoto wa Tanzania.

Ripoti hii inatoa makadirio ya kwanza ya ukubwa na sura ya ukatili wa kijinsia, kimwili na kiakili yanayowasibu wasichana na wavulana Tanzania. Matokeo ya uchunguzi huu yatasaidia juhudi za kuweka mikakati madhubuti ya kuzuia na kukabili na kuanzisha taratibu za kuboresha huduma kwa watoto waathirika wa ukatili. Kwa kuwa hakuna mfumo wa kitaifa wa kuwalinda watoto, ni muhimu kwa Tanzania kubuni taratibu na michakato yenye nguvu za kisheria inayotekelezeka na ya kuwapatia huduma ya kuwalinda watoto dhidi ya ukatili kama ilivyoelezwa katika ripoti hii. Kwa lengo hilo, matokeo ya Utafiti wa Tanzania yanatoa ushahidi makini na madhubuti kwa ajili ya kuandika miongozo na kanuni zinazohusu utekelezaji wa Sheria ya Mtoto Na 21 ya 2009.

Utafiti waUkatili Dhidi ya Watoto Tanzania uliongozwa na Kikosi Kazi Kinachojumuisha Sekta Mbalimbali (KKKSM), kikishirikisha wawakilishi wa wizara za serikali na washirika wakiwemo: sekta ya polisi na sheria; sekta za ustawi wa jamii, elimu na afya; umoja wa mataifa na asasi za kiraia. Mwenyekiti wa KKKSM ni Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto (WMJJW) na Kikosi Kazi kinahakikisha uwajibikaji kitaifa na usimamizi katika kubuni Mpango wa Taifa wa Kuzuia na Kukabiliana na matokeo ya Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania (UDWT)

Madhumuni ya UDWT 2009 yalikuwa:

- kuelezea ukubwa wa tatizo la ukatili dhidi ya watoto chini ya umri wa miaka 18 Tanzania na kumulika hasa ukatili ya kijinsia
- kuainisha yanayoweza kuchangia kusababisha au kuzuia ukatili dhidi ya watoto.
- kuainisha athari za kiafya za ukatili dhidi ya watoto.
- kutathmini matumizi ya huduma za kijamii, sheria ya jinai na huduma za afya na watoto wanaofanyiwa ukatili
- kutumia takwim kuongoza sera na mipango ya kuzuia na kuwalinda watoto dhidi ya ukatili.

Matokeo yanatolewa hapa ni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (yaani Tanzania bara na Zanzibar kwa pamoja). Matokeo ya Zanzibar yanajadiliwa kwa kina peke yake kwenye ripoti tofauti, na Zanzibar itandaa mpango wake yenyewe wa kuzuia na kukabiliana na ukatili, ikiongozwa na KKKSM Zanzibar. Hivyo, takwimu katika ripoti hii ni za Tanzania bara pamoja na Zanzibar isipokuwa pale tu ilipoashiriwa vinginevyo. Data zilikusanywa kutoka wasichana na wavulana wenye umri kati ya miaka 13 na 24, ambao waliripoti ukatili uliowasibu kabla hawajatimiza miaka 18.

Matokeo yanaonyesha umuhimu wa kupambana na ukatili dhidi ya watoto kwa haraka katika sekta zote na katika maeneo ambayo watoto hutumia muda mwingi, hususan majumbani mwao, katika jamii na shuleni. Hali endelevu ya kujituma ya KKKSM itahakikisha kwamba matokeo yanasikika, yanasambazwa, na kufanyiwa kazi barabara kwa ushirikinao wa wizara zote husika na washirika.

Uwajibikaji wa dhati wa wadau wote hatimae utainufaisha Jamhuri ya Muunganao wa Tanzania kwa:

- kupunguza kuenea kwa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto
- kuboresha upatikanaji na viwango vya huduma kwa waathirika wa vitendo vya ukatili
- kupunguza makali ya athari za kiafya zitokanazo na vitendo hivyo vya ukatili na
- kuzithibitisha haki na heshima za watoto wote wa Tanzania.

[a] Ukatili wa kijinsia ulikuwa ndio msingi wa utafiti kwa sababu wadau Tanzania walianisha kama tatizo zito.

2. Kuenea kwa Ukatili wa kijinsia, kimwili na kiakili Tanzania.

Picha: UNICEF/Giacomo Pirozzi

2. Kuenea kwa Ukatili wa kijinsia, kimwili na kiakili Tanzania.

DONDOO KUU

- Takriban wasichana 3 kati ya 10 na mvulana 1 kati ya 7 waliripoti walau tukio moja la kufikwa na ukatili wa kijinsia kabla ya kutimiza umri wa miaka 18.
- Karibu asilimia 6 ya wasichana walilazimishwa kufanya ngono kabla ya kufikia miaka 18.
- Takriban robo tatu ya watoto –wasichana kwa wavulana- walitendewa ukatili wa kimwili kabla ya kutimiza miaka 18.
- Takriban robo ya watoto- wasichana kwa wavulana- walitendewa ukatili wa kiakili kabla ya kutimiza miaka 18.

Makadirio ya kuenea kwa na aina za ukatili wa kijinsia, kimwili na kiakili nchini Tanzania dhidi ya watoto yanaonyesha kuna tatizo kubwa: takriban asilimia 28 ya wasichana na asilimia 13 ya wavulana wamefikwa na ukatili wa kijinsia kabla ya kutimiza miaka 18, zaidi ya asilimia 70 ya wasichana na wavulana wametendewa ukatili wa kimwili na zaidi ya robo wametendewa ukatili wa kiakili (angalia Mchoro 1).

Mchoro 1: Ukatili wa kijinsia, kimwili na kiakili uliotokea utotoni. Taarifa za wenye umri wa miaka 13 hadi 24 (Ripoti ya Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania 2009 - RUDWT 2009)



Ukatili wa Kijinsia Utotoni

Ukatili wa kijinsia Tanzania ni tatizo kubwa la afya ya jamii na haki za binadamu linalohitaji hatua za mara moja nchini kote. Wasichana na wavulana wa Kitanzania walitakiwa kutoa maelezo ya ukatili wa kijinsia yaliowafika kabla hawajatimiza umri wa miaka 18. Vilevile waliulizwa walikuwa na umri gani wakati kila tukio lilipotokea, na yalitokea baada ya muda gani. Vitendo vya ukatili wa kijinsia ni:

- **kuguswa bila ridhaa** kijinsia (yaani, kuguswa sehemu usiyotaka, kupigwa busu, kushikwa au kutomaswa)
- **jaribio la kujaamiiana** ambalo mkosaji alijaribu kufanya ngono lakini bila mafanikio
- **kufanya ngono** kulilazimishwa kwa kutumia nguvu, na
- **Kujamiiana kwa kushurutishwa** ambapo shinikizo na vitisho vinatumika kulazimisha kujamiiana.

Viwango vya ukatili wa kijinsia viko juu. Katika kipindi cha miezi kumi na mbili kabla ya utafiti, asilimia 6 ya wavulana wa Kitanzania wenye umri wa miaka kati ya 13 na 17 walifikwa na walau tukio moja la ukatili wa kijinsia. Kiwango kilikuwa zaidi ya mara mbili kwa wasichana wa Tanzania, asilimia 14. Huko Zanzibar mwelekeo ulikuwa kinyume kijinsia; asilimia 2 ya wasichanana na asilimia 4 ya wavulana wenye miaka kati ya 13 na 17 waliripoti kutendewa ukatili katika mwaka uliyopita.

Kati ya hao waliokumbwa na ukatili wa kijinsia, takriban wasichana 4 kati ya 10 na wavulana 3 kati ya 10 walikumbwa na matukio zaidi ya matatu kabla ya kufikisha umri wa miaka 18. (angalia Mchoro 2).

Mchoro 2: Asilimia ya wenye miaka 13 hadi 17 waliotendewa ukatili wa kijinsia mara nyingi. Taarifa ya wenye umri wa miaka 13 hadi 17 waliofanyiwa ukatili wa kijinsia (RUDWT 2009)



Wasichana na wavulana wa Kitanzania walisema aina ya ukatili wa kijinsia iliyokuwa ya kawaida zaidi ilikuwa kuguswa kijinsia, ikifuatiwa na jaribio la kujamiiana, (angalia Mchoro 3). Hususan, takriban asilimia 7 ya wasichana na takriban asilimia 3 ya wavulana walilazimishwa au kushurutishwa kufanya ngono kabla hawajatimiza miaka 18. Lakini Zanzibar kwa wasichana jaribio la kufanya ngono lilikuwa ni tukio lililotokea zaidi kwa ukatili wa kijinsia, likifuatiwa na kuguswa bila ridhaa.

Mchoro 3: Aina ya Ukatili wa Kijinsia uliotokea utotoni kabla ya kutimiza umri wa miaka 18. Taarifa ya wenye umri wa miaka 13 hadi 24 (RUDWT 2009)



Waathirika ni wa umri mbalimbali. Ukatili wa kijinsia unawasibu watoto wa kila umri. Takriban asilimia 20 ya wasichana waliripoti kitendo cha kufanya ngono mara ya kwanza kilikuwa cha ukatili wa kijinsia wa aina moja au nyingine kabla ya kutimiza miaka 14; asilimia 40 ya wasichana walikuwa na miaka kati ya 14 na 15; na wengine asilimia 40 walikuwa kati ya miaka 16 na 17 walipofanyiwa tendo la kwanza la ukatili wa kijinsia (angalia Mchoro 4). Wavulana walielekea kufikwa na ukatili wa kijinsia wakati wakiwa na umri mkubwa zaidi. Takribani asilimia 16 ya wavulana walifanyiwa ukatili wa kijinsia wakati wakiwa na miaka chini ya 14, takriban asilimia 27 walikuwa na umri kati ya miaka 14 na 15; na takriban asilimia 60 walikuwa kati ya miaka 16 na 17.

Mchoro 4: Umri wakati tukio la kwanza la ukatili wa kijinsia lilitokea utotoni. Taarifa za wenye umri wa miaka 18 hadi 24 waliofanyiwa ukatili wa kijinsia utotoni (RUDWT 2009)



Mara nyingi tendo la kwanza la kujamiiana si la ridhaa. Asilimia kubwa kiasi ya wavulana na wasichana wa Kitanzania walisema hawakutaka kushiriki katika tukio la kwanza la kujamiiana (asilimia 18 wavulana na asilimia 29 wasichana); Zanzibar, asilimia 10 ya wavulana na wasichana walisema hawakuridhia tendo lao la kwanza la kujamiiana. Miongoni mwao waliofanya ngono kwa mara ya kwanza bila ridhaa yao, wasichana 5 kati ya 10 na wavulana 6 kati ya 10 walisema walighilibiwa.

Ukatili wa kimwili utotoni

Wasichana na wavulana waliulizwa kuhusu ukatili wa kimwili uliowasibu kama vile kuzabwa kofi, kusukumwa, kupigwa ngumi, kupigwa teke, kupigwa, au kuvamiwa au kutishiwa na silaha kama bunduki au kisu. Zaidi ya nusu ya wavulana na wasichana wenye umri kati ya miaka 13 na 17 waliripoti waliwahi kufikwa na ukatili wa aina hii uliofanywa na ndugu, mtu mwenye mamlaka juu yake au mwandani wake.

Matukio ya ukatili wa kimwili ni mengi zaidi kuliko matukio ya ukatili wa kijinsia. Zaidi ya asilimia 73 ya wasichana na takriban asilimia 72 ya wavulana walikuwa waathirika wa ukatili wa kimwili. Kupigwa ngumi, kuchapwa, na kupigwa teke ndiyo aina za matendo ya kutumia nguvu kimwili yaliyowasibu (angalia Mchoro 5). Takriban asilimia 3 ya wasichana na wavulana waliripoti kutishiwa na silaha utotoni mwao.

Mchoro 5: Aina ya ukatili wa kimwili. Taarifa ya wenye miaka 13 hadi 24 waliofanyiwa ukatili wa kimwili utotoni (RUDWT 2009)



Ukatili wa kiakili utotoni

Vitendo kama kuitwa majina mabaya, kufanywa ujisikie hutakiwi au kutishiwa kutelekezwa na watu wazima au mwandani (lakini si marafiki au wenzako) ni mifano ya ukatili ya kiakili.

Robo ya watoto wanafanyiwa ukatili wa kiakili. Takriban robo ya watoto wa Kitanzania, wavulana kwa wasichana, walisema wameshawahi kufanyiwa ukatili ya kiakili, kuitwa majina mabaya ilikuwa aina ya tukio la ukatili wa kiakili lilotokea mara nyingi zaidi (liliwasibu asilimia 22 ya wavulana na asilimia 18 ya wasichana, angalia Mchoro 6). Takriban asilimia 9 ya wasichana na asilimia 7 ya wavulana walisema walijisikia hawatakiwi, wakati asilimia 4 ya wasichana na asilimia 5 ya wavulana walitishiwa kutelekezwa kabla ya kutimiza miaka 18.

Mchoro 6: Aina za Ukatili wa kiakili utotoni. Taarifa za wenye umri wa 13 hadi 24 (RUDWT 2009)



Mwingiliano wa aina ya ukatili

Watoto walio wengi wanakabiliwa na mchanganyiko wa mazingira hatarishi. Uhusiano na mwingiliano kati ya aina ya ukatili unaashiria hatari nyingi zinazowazunguka watoto wa Tanzania. Zaidi ya watoto 8 kati ya 10 wasichana na wavulana, waliofanyiwa ukatili wa kijinsia, pia walifanyiwa ukatili wa kimwili, wakati wasichana 4 kati ya 10 na wavulana 5 kati ya 10 walifanyiwa ukatili wa kiakili (angalia Mchoro7). Mchanganyiko huu wa aina za ukatili utotoni unaonyesha umuhimu wa kukabiliana na hali mbalimbali hatarishi zinazowakabili watoto wa Kitanzania.

Mchoro 7: Waathirika wa ukatili wa kijinsia ambao pia walifanyiwa ukatili wa kimwili na kiakili. Taarifa za wenye umri wa miaka 13 hadi 24 (RUDWT 2009)



Uhusiano kati ya ukatili wa kimwili na kiakili
Watoto walio wengi zaidi ambao wamewahi kufanyiwa ukatili wa kimwili pia walifanyiwa ukatili wa kiakili. Ukatili wa kiakili uliwakumba asilimia 9 ya wasichana na asilimia 14 ya wavulana.

Yatima wako katika hali hatarishi zaidi. Umasikini, kupanuka kwa miji, kumomonyoka kwa maadili na desturi za familia, na athari za janga la UKIMWI/VVU vinaashiria kwamba watoto ambao hawako katika utamaduni wa kuishi kifamilia na kijamii wako katika hali hatarishi ya kukumbwa na ukatili. Ripoti ya Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania (RUDWT) 2009 ilikadiria kwamba zaidi ya robo ya wasichana na zaidi ya moja ya tano ya wavulana walikuwa yatima, kwa maana ya mtu aliyefiwa na mzazi mmoja au wote wawili kabla ya kutimiza miaka 18. RUDWT haikujumuisha taarifa za watoto wanaoishi katika taasisi za kutunza yatima au wasioishi nyumbani, hilo ni eneo ambalo linastahili utafiti zaidi kuhusu unyanyasaji na ukatili.

Yatima wako katika hatari zaidi ya kukumbwa na ukatili kuliko wasio yatima. Ukatili wa kijinsia uliowakumba watoto kabla ya miaka 18 asilimia 36 ya wasichana walikuwa yatima ukilinganisha na asilimia 25 ya wasichana ambao hawakuwa yatima, na ukatili wa kiakilia utotoni uliwakumba wasichana yatima asilimia 31 ukilinganisha na asilimia 21 ya wasichana wasio yatima. Wavulana waliopoteza mama zao kabla ya kufika umri wa miaka 18 walikumbwa zaidi na ukatili wa kiakili kuliko wale wasio kuwa yatima (asilimia 44 ya wavulana yatima ukilinganisha na asilimia 26 wasiokuwa yatima).

3. Ukatili Dhidi ya Watoto: ni nani, wapi na wakati gani?

Picha: UNICEF/Shehzad Noorani

3. Ukatili Dhidi ya Watoto: ni nani, wapi na wakati gani?

DONDOO KUU

- Wandani, majirani, na watu wasiofahamika, walitajwa zaidi kama wakosaji kwa ukatili wa kijinsia.
- Wakosaji wengi wa ukatili wa kijinsia dhidi ya wasichana walikuwa wana umri mkubwa kuliko waathirika, wakati wakosaji wa ukatili wa kijinsia dhidi ya wavulana walikaribiana umri na muathirika.
- Takriban watoto 6 kati ya 10 wasichana na wavulana walifanyiwa ukatili wa kimwili na ndugu na 1 kati ya 2 walifanyiwa na waalimu.
- Ndugu na majirani ndiyo waliokuwa watendaji wakubwa wa ukatili wa kiakili
- Vitendo vya ukatili wa kijinsia utotoni vilitokea zaidi nyumbani kwa mtu na shuleni au njiani kwenda au kutoka shule.
- Wasichana waliokumbwa na ukatili wa kijinsia kwa kushurutishwa au kulazimishwa kujamiiana ilikuwa nyumbani kwa mkosaji.
- Matukio yaliyo mengi ya ukatili wa kijinsia dhidi ya wasichana na wavulana yalitokea kati ya adhuhuri na saa 2 usiku.

Katika jitihada za kuzuia ukatili dhidi ya watoto, ni muhimu wakosaji watambuliwe mapema. Taarifa kuhusu aina ya watu wanaofanya vitendo vya ukatili kwa watoto kijinsia, kimwili na kiakili zinaweza kutumika kubaini ni vipi, wapi, wakati gani na katika mazingira gani vitendo vya ukatili vinafanyika. Vielelezo hivi ni uthibitisho muhimu unaoweza kutumika kulenga na kupanga sera na mikakati ya kitaifa za kuzuia na kukabiliana na matatizo haya.

Wakosaji wa ukatili wa kijinsia, kimwili na kiakili mara nyingi wako karibu na wanafahamika na watoto. Ukatili ya kijinsia hutokea nyumbani kwa mkosaji au muathirika au wakati mtoto yuko njiani kwenda au kutoka shule. Matendo mengi ya ukatili wa kijinsia kwenye sehemu ambazo ingedhaniwa watoto wangekuwa salama, inaonyesha usiri wa vitendo vya ukatili wa kijinsia, na ni changamoto kubwa kwa juhudi za kuzuia na kukabiliana na tatizo hili nchini Tanzania.

Ni nani wanaofanya ukatili wa kijinsia?

Wasichana na wavulana waliofanyiwa ukatili wa kijinsia waliulizwa swali mahususi kuhusu matukio ya ukatili wa kijinsia. Waliwataja wakosaji, walitaja ukatili ulitendeka wapi, na kulielezea kila tendo lilikuaje. Matokeo yamelenga kwenye idadi ya wasichana na wavulana waliokumbwa na ukatili wa kijinsia na nani mhusika, wapi tukio lilitokea, wakati na sehemu. Kwa mfano, kuna matukio, msichana anakumbwa na ukatili wa kijinsia shuleni na nyumbani.

Waathirika mara nyingi waliwafahamu waliowatendea ukatili. Kwa wasichana waliotoa taarifa ya ukatili wa kijinsia utotoni, karibia theluthi moja walisema katika tukio moja mkosaji alikuwa ni jirani, na theluthi nyingine walisema mkosaji alikuwa mtu asiyejulikana, na robo walitoa taarifa mkosaji alikuwa mwandani wake. Takriban msichana 1 kati ya 10 alitoa taarifa tukio moja mkosaji alikuwa mwalimu, wakati asilimia saba walisema mkosaji alikuwa ndugu mjomba au binamu. Takriban mvulana 1 kati ya 2 wakiokumbwa na ukatili wa kijinsia walisema mkosaji wa tukio moja alikuwa mndani wake, na robo walisema mkosaji alikuwa mtu asiyejulikana. Takriban asilimia 17 ya wavulana walisema jirani alikuwa mkosaji wakati asilimia 14 ya wavulana walisema ndugu, na 11 kati ya hao wavulana 26 walisema mkosaji alikuwa ndugu wa kike.

Jedwali 1: Wakosaji wa ukatili ya ngono kama ilivyoripotiwa na wenye umri kati ya 13 na 24 (RUDWT 2009)		
Mshambuliaji wa kijinsia	**Wasichana**	**Wavulana**
Jirani	32.2 %	16.6 %
Mtu asiyejulikana	32.0 %	25.7 %
Mwandani	24.7 %	47.9 %
Mtu mwenye mamlaka juu ya mhanga	14.7 %	2.8 %
Rafiki/mwanafunzi mwenzie wa darasa moja	10.3 %	8.6 %
Ndugu	7.1 %	14.1 %

Watendaji ukatili wa kijinsia mara nyingi ni wakubwa kuliko waathirika. Bila kujali aina ya ukatili wa kijinsia (k.m. kulazimisha/kushurutishwa, kugusa, jaribio la kujamiiana) takriban wasichana 7 kati ya 10 waliripoti mkosaji alikuwa na umri mkubwa zaidi yao, na 4 kati ya 10 walisema mkosaji aliwazidi walau kwa miaka 10 kiumri (angalia Mchoro 8). Taarifa za wavulana zilitofautiana na za wasichana, walisema mkosaji alikuwa hapishani nao kiumri, pale ambapo tendo lilikuwa kushika bila ridhaa au jaribio la kufanya ngono. Kwenye ukatili wa kulazimisha au kushurtisha ngono au kujamiiana theluthi mbili za wavulana walitoa taarifa mkosaji alikuwa amewazidi umri.

Mchoro 8: Tofauti ya umri kati ya mkosaji na muathirika wa kike wa ukatili wa kijinsia utotoni. Taarifa za wenye miaka 13 hadi 24 waliofanyiwa ukatili wa kijinsia utotoni (RUDWT 2009)[a]



[a]Jumla ya asilimia ni kubwa kuliko 100 kwa sababu wasailiwa waliotoa taarifa ya zaidi ya matukio nane, ambayo yangeweza kuwa ni ya wakosaji mbali mbali.

Utumiaji nguvu ni kawaida. Takriban robo tatu ya wasichana na nusu ya wavulana ambao walifanyiwa ukatili wa kijinsia walisema nguvu au tishio la kutumia nguvu zilitumiwa na wakosaji kutekeleza kujamiiana bila ridhaa, jaribio la kujamiiana au kufanikisha kujamiiana. Washambuliaji walitumia nyanyaso, uongo, au ghilba dhidi ya asilimia 28 ya wasichana na asilimia 19 ya wavulana (angalia Mchoro 9).

Mchoro 9: Aina ya nguvu au ushurutishaji uliotumika katika tukio au jaribio la kwanza la ngono ya kulazimishwa utotoni. Taarifa ya wenye umri miaka 13 hadi 24. (RUDWT 2009)



Matendo mengi ya ukatili hayakusababishwa na uchokozi. Ili kuelewa vizuri zaidi mazingira ya matukio, wasailiwa waliulizwa ni nini kilikuwa kinaendela mara kabla ya tukio. Wengi, takriban nusu ya wasichana na nusu ya wavulana walisema hakuna kitu maalum kilikuwa kinafanyika, lakini asilimia 17 ya wasichana walisema walikuwa wanabishana na mkosaji wao kabla ya tukio la ukatili wa kijinsia kutokea, na zaidi ya asilimia 9 walisema walikuwa kwenye miadi wakati wa tukio au kabla ya tukio.

Ni nani wanaotenda ukatili wa kimwili?

Kwa ujumla, takribani robo tatu ya wasichana na wavulana kati ya miaka 13 na 24 walifanyiwa ukatili wa kimwili kabla hawajatimiza miaka 18. Kwa kiasi kikubwa wakosaji walikuwa ndugu za watoto au waalimu.

Mchoro 10: Watendaji wa ukatili wa kimwili kwa utotoni. Taarifa za wenye miaka 13 hadi 24. (RUDWT 2009)[a]



[a]Asilimia ni kubwa kuliko 100 kwa sababu wasailiwa walitoa taarifa ya matukio mengi yaliyowahusu wakosaji mbalimbali.

*Makadirio sio kamilifu.

Watoto walikuwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kupigwa (kupigwa ngumi, kuchapwa, kupigwa teke) na ndugu zao. Karibu asilimia 60 ya wasichana na wavulana wa Kitanzania waliotoa taarifa ya kupigwa walipigwa na ndugu. Wazazi waliongoza kama wakosaji wakuu wa ukatili wa kimwili dhidi ya watoto wao, na kulikuwa na uwezekano mkubwa zaidi wa mtoto wa kike kupigwa na mama yake na uwezekano mkubwa zaidi wa mvulana kupigwa na baba yake (angalia Jedwali 2).

Jedwali 2: Kuenea kwa ukatili ya kimwili ya ndugu dhidi ya watoto kama ilivoripotiwa na wenye miaka 13 na 24 (AMNUDW 2009)		
Mshambuliaji kimwili	**Wasichana**	**Wavulana**
Baba	36.9 %	50.9 %
Mama	49.3 %	36.0 %
Kaka	12.2 %	15.2 %
Dada	9.2 %	3.4 %
Mjomba, Baba mdogo au mkubwa/ Shangazi, Mama mdogo au mkubwa	9.3%	15.1%
Ndugu mwingine	5.5 %	5.9 %

Unyanyasaji nyumbani ni kawaida na hutokea mara nyingi. Katika maisha ya utoto, wasichana na wavulana wengi walisema waliwahi kupigwa na ndugu zaidi ya mmoja. Kwa mfano, asilimia 24 ya wasichana na asilimia 23 ya wavulana wa Kitanzania walipigwa na ndugu wawili, wakati asilimia 9 ya wasichana na asilimia 11 ya wavulana walipigwa na ndugu watatu au zaidi.

Wingi wa matukio ya kupigwa na ndugu ni muhimu: takriban asilimia 46 ya wasichana kwa wavulana wa Kitanzania walionyanyaswa walipigwa ngumi, walipigwa teke, au walichapwa zaidi ya mara tano utotoni (angalia Mchoro 11). Takriban 3 kati ya 10 walitoa taarifa kwamba walipigwa ngumi, walipigwa teke au walichapwa mara moja au mbili.

Mchoro 11: Idadi ya matukio wenye umri wa miaka 13 hadi 17 walitoa taarifa za kupigwa ngumi, kupigwa teke na kuchapwa na ndugu. (RUDWT 2009)



Waalimu pia ni wanyanyasaji wakubwa. Ukatili wa kimwili umeenea sana miongoni mwa waalimu. Zaidi ya nusu ya wasichana na wavulana wa Kitanzania waliwataja waalimu kama wanyanyasaji. Kati ya watoto walionyanyaswa na waalimu asilimia 56 ya wasichana na asilimia 48 ya wavulana walisema walifanyiwa ukatili wa kimwili na waalimu wa kike na wa kiume. Theluthi ya wasichana walisema walifanyiwa ukatili na waalimu wa kiume tu, asilimia 12 walitoa taarifa walifanyiwa ukatili na waalimu wa kike tu (angalia Jedwali 3). Wakati huo huo asilimia 46 ya wavulana walitoa taarifa kufanyiwa ukatili wa kimwili na waalimu wa kiume tu, na asilimia 6 walitoa taarifa walifanyiwa ukatili wa kimwili na waalimu wa kike tu.

Jedwali 3: Kuenea kwa ukatili wa kimwili miongoni mwa waalimu wa kike na wa kiume kama ilivyoripotiwa na wenye miaka kati ya 13 na 24 waliowataja waalimu kama washambuliaji (RUDWT 2009)

	Wasichana	Wavulana
Kunyanyaswa na walimu wa kike na wa kiume	55.9 %	48.1 %
Kunyanyaswa na walimu wa kiume tu	31.9 %	46.2 %
Kunyanyaswa na walimu wa kike tu	12.2 %	5.8 %

Kuenea kwa unyanyasaji miongoni mwa waalimu ni kwa hali ya juu inayotisha: asilimia 78 ya wasichana na asilimia 67 ya wavulana walitoa taarifa ya kufanyiwa ukatili na waalimu walisema walipigwa ngumi, walipigwa teke au walichapwa zaidi ya mara tano na mwalimu kabla ya kutimiza miaka 18. (angalia Mchoro 12).

Mchoro 12: Idadi ya matukio kwa wenye umri wa miaka 13 hadi 17 walito taarifa za kupigwa ngumi, kupigwa teke na kuchapwa na mwalimu. (RUDWT 2009)



Ni nani wanaofanya ukatili wa kiakili?

Ndugu na majirani ni wanyanyasaji wa kiakili. Kwa kiasi kikubwa wanyanyasaji wa kiakili walikuwa ni ndugu za mtoto. Takriban asilimia 80 ya wasichana wa Kitanzania na asilimia 65 ya wavulana wa Kitanzania waliokumbwa na ukatili wa kiakili walisema ndugu ndiye aliyekuwa mkosaji (angalia Mchoro 13). Wanyanyasaji waliofuatia ni majirani, msichana 1 kati ya 5 na takriban mvulana 1 kati ya 3 waliwataja majirani kama wanyanyasaji wa kiakili. Mara nyingi watoto walinyanyaswa kiakili na wakosaji aina nyingi: asilimia 42 ya wasichana na asilimia 38 ya wavulana walisema walinyanyaswa kiakili na zaidi ya mkosaji wa aina moja.

Mchoro 13: Waliotenda ukatili wa kiakili kwa watoto. Taarifa za waathirika wa ukatili wa kiakili wenye miaka 13 hadi 24. (RUDWT 2009)[a]



[a]Asilimia imezidi 100 kwa sababu wasailiwa walitoa taarifa ya wakosaji wa aina nyingi.

Watoto huwa hatarini zaidi wapi na wakati gani?

Pamoja na kujua wakosaji ni akina nani ni muhimu kujua ni wapi na ni wakati gani na kwa jinsi gani ukatili unafanyika ili kusaidia jitihada za kuzuia ukatili. Kwa hiyo wasichana na wavulana waliulizwa kuhusu taarifa ya eneo ukatili wa kijinsia ulitendeka na saa ngapi.

Matendo mengi ya Ukatili wa kijinsia yanatokea nyumbani au shuleni. Wasichana na wavulana wa Kitanzania walisema karibu nusu ya matukio ya ukatili wa kijinsia yalifanyika kwenye nyumba ya mtu (angalia Jedwali 4). Hili linashabihiana na taarifa ya kwamba mshambuliaji mara nyingi alikuwa mtu anaefahamika na muathirika. Pia, shuleni au njiani kwenda shule zilikuwa ni sehemu kuu hatarishi za ukatili wa kijinsia. Takriban robo ya wasichana na wavulana walisema kwamba walau tukio moja la ukatili wa kijinsia lilitokea kiwanjani, kichakani, mtoni au barabarani, wakati msichana 1 kati ya 10 na mvulana 1 kati ya 20 walitaja matukio kwenye jengo la hadhara kama kwenye biashara au baa.

Jedwali 4: Mahali pa matukio ya ukatili wa kijinsia yaliyotokea utotoni kwa wasailiwa wenye miaka kati ya 13 na 24 (RUDWT 2009)

	Wasichana	Wavulana
Nyumbani kwa mtu	49.0 %	45.7 %
Uwanjani/kichakani/mtoni/barabarani	24.2 %	26.7 %
Kuelekea/kutoka shule	23.0 %	15.3 %
Shuleni	15.1 %	13.3 %
Jengo la hadhara	10.0 %	4.5 %
Kwingineko	5.8 %	6.8 %

Ukatili wa aina tofauti hutokea sehemu tofauti

Kujamiiana kwa kulazimishwa au kushurtishwa
Kitendo cha ngono ya kulazimishwa au kushurtishwa kwa wasichana kulitokea zaidi nyumbani kuliko ukatili wa kijinsia wa aina nyingine. Kwa mfano, takriban wasichana 3 kati ya 4 waliotoa taarifa ya kukumbwa na tendo la ngono ya kulazimishwa au kushurtishwa walisema walau tukio moja lilkuwa nyumbani kwa mtu. Kati ya waliotoa taarifa ya kulazimishawa au kushurtishwa kufanya ngono nyumbani kwa mtu, asilimia 70 walisema ilikuwa nyumbani kwa mkosaji.

Matokeo ya wavulana wa Kitanzania yalifanana na wasichana: asilimia 61 ya wavulana walisema walifikwa na tukio la ngono ya kulazimishwa au kushurtishwa nyumbani kwa mtu; asilimia 50 ya matukio yalitokea nyumbani kwa mvulana mwenyewe. Wavulana wa Kitanzania walisema kushikwa bila ridhaa na majaribio ya kujamiiana yalitokea shuleni na nyumbani (asilimia 45 na 29, mtawalia).

Kuguswa bila ridhaa au jaribio la kujamiiana
Asilimia arobaini na tatu ya wasichana walisema walau tukio moja la kuguswa bila ridhaa au jaribio la kujamiiana lilitokea nyumbani. Aina tatu za nyumba ambazo zilitajwa zaidi kuwa tukio moja lilitokea zilikuwa: nyumbani kwa mtoto mwenyewe (asilimia 45), nyumbani kwa mkosaji (asilimia 37) na nyumba nyingine (asilimia 29), kwa mfano nyumbani kwa rafiki, ndugu au jirani. Zaidi ya asilimia 41 ya wasichana walishikwa bila ridhaa walau mara moja au kufikwa na jaribio la kujamiiana wakiwa shule (asilimia 17) au wakiwa njiani kwenda au kutoka shule (asilimia 26).

Matukio mengi ya Ukatili wa kijinsia hutokea adhuhuri mpaka saa mbili usiku. Zaidi ya asilimia 40 ya wasichana na asilimia 35 ya wavulana waliokumbwa na ukatili wa kijinsia walitoa taarifa kuwa tukio moja lilitokea kati ya adhuhuri na saa kumi na moja jioni. Zaidi ya theluthi moja ya wasichana na wavulana walisema ukatili wa kijinsia ulitokea kati ya saa kumi na moja jioni na saa mbili usiku. Wachache sana walitoa taarifa ya kukumbwa na ukatili wa kijinsia usiku wa manane hadi saa moja asubuhi.

Mchoro 14: Muda katika siku ambapo tukio la kwanza la ukatili wa kijinsia lilifanyika dhidi ya wasichana kama ilivyoarifiwa na wenye miaka 13 hadi 24 (RUDWT 2009)



4. Athari za ukatili dhidi ya watoto: kwa nini ni muhimu

Picha: UNICEF/Hiroki Gomi

4. Athari za ukatili dhidi ya watoto: kwa nini ni muhimu

DONDOO KUU

Utoaji taarifa na majibu

- Takriban nusu ya wasichana na theluthi ya wavulana waliokumbwa na ukatili wa kijinsia kabla ya kutimiza miaka 18 walitoa taarifa kwa mtu.
- Takriban msichana 1 kati ya 5 na mvulana 1 kati ya 10 walitafuta huduma kwa yale yaliyowasibu kufuatia ukatili wa kijinsia kabla ya kutimiza miaka 18.
- Takriban msichana 1 kati ya 8 na mvulana 1 kati ya 20 walipata huduma kwa yaliyowasibu kutokana na ukatili wa kijinsia kabla ya kutimiza miaka 18.
- Takriban asilimia 16 ya wasichana na wavulana waliokumbwa na ukatili wa kijinsia kabla ya kutimiza miaka 18 wangelipenda kuweza kupata msaada zaidi.

Athari za ukatili wa kijinsia

- Kwa wasichana wa miaka kati ya 13 na 24, kujisikia kuwa na hofu na msongo wa mawazo katika siku 30 zilizopita, unywaji wa pombe katika siku za karibuni na kuambukizwa magonjwa ya zinaa au kuwa na dalili ya maambukizo hayo katika miezi 12 iliyopita vyote vilihusishwa na ukatili wa kijinsia utotoni.
- Zaidi ya asilimia sita ya wasichana wenye miaka kati ya 13 na 24 ambao waliwahi kupata mimba walisema ujauzito mmoja ulisababishwa na ukatili wa kijinsia.
- Kutotumia kondomu kabisa au kutotumia mara kwa mara katika kipindi cha miezi 12 iliyopita ilikuwa kawaida zaidi miongoni mwa vijana, wake kwa waume, wenye miaka kati ya 19 na 24 wenye historia ya kukumbwa na ukatili wa kijinsia utotoni kuliko wale ambao hawakuwa na historia ya ukatili wa kijinsia.
- Tabia ya kujamiiana na watu wawili au zaidi katika miezi 12 iliyopita ilikuwa juu zaidi miongoni mwa wanawake na wanaume vijana wenye umri kati ya miaka 19 hadi 24 wenye historia ya kukumbwa na ukatili wa kijinsia utotoni kuliko wale ambao hawakuwa na historia ya ukatili wa kijinsia.
- Msichana 1 kati ya 25 mwenye umri wa miaka 13 hadi 17 amewahi kupewa pesa au zawadi ili afanye ngono. Matendo ya ukatili utotoni ya kijinsia, kimwili na kiakili yalikuwa mengi zaidi kwa wasichana wenye miaka kati ya 13 na 17 ambao walitoa taarifa ya kupokea pesa au zawadi ili wafanye ngono ikilinganishwa na wale ambao hawakupokea pesa wala zawadi ili wafanye ngono.

Athari za ukatili wa kimwili

- Kwa wanawake wenye miaka kati ya 13 na 24, matukio ya ukatili wa kimwili utotoni yalihusishwa na afya mbaya au ya wastani, kuwa na hofu katika siku 30 zilizopita, kuwa na mawazo ya kujiua, na kupatikana na magonjwa ya zinaa au dalili zake katika miezi 12 iliyopita.
- Kwa wanaume wenye miaka kati ya 13 na 24, ukatili wa kimwili utotoni ulihusishwa kwa mbali na kuwa na msongo wa mawazo katika siku 30 zilizopita.

Athari za ukatili wa kiakili

- Kwa wanaume na wanawake wenye miaka 13 na 24, ukatili wa kiakili utotoni ulihusishwa na afya mbaya au ya wastani, kuwa na hofu au msongo wa mawazo katika siku 30 zilizopita, na kuwa na mawazo ya kujiua.

Utafiti wa kimataifa umeonyesha kwamba matatizo mengi ya kiakili na tabia katika ujana na utu uzima yanahusiana na kukumbwa na ukatili utotoni. Haya ni pamoja na tabia ya ugomvi, kutowajibika, tabia mbaya, matumizi ya dawa za kulevya, matokeo mabaya ya masomo, kupata kiwewe, hofu, msongo wa mawazo, kujiona huna thamani na tabia ya mtu kuhatarisha maisha yake mwenyewe. Athari zinaweza kupishana kutegemeana na umri wa mtoto alipokuwa muathirika, kiwango cha ukatili na ukatili ulikuwa wa muda gani, ustahimilivu wa mtoto mwenyewe na vigezo vingine. Hususan, ukatili wa kijinsia unahusishwa na hatari ya kupata matatizo ya kijinsia na ya kizazi, na uambukizaji wa UKIMWI na maambukizo mengine ya magonjwa ya zinaa.

Wasichana na wavulana wa Kitanzania waliulizwa maswali mbalimbali kuhusu hali zao kimwili na kiakili pamoja na ufahamu wao, msimamo wao, na tabia zao kuhusu kujamiiana, VVU na ukatili wa kimwili. Mahusianao mengi yaliyotajwa hapo juu kuhusu ukatili wa kijinsia yalidhihirika miongoni mwa Watanzania waliokumbwa na ukatili utotoni.

Ukatili utotoni na uwezo wa kutafuta msaada.

Watoto wanaokumbwa na ukatili wa kijinsia mara nyingi hawapendi kuwaeleza wengine kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kujiona wana makosa, aibu, uoga wa kutoaminiwa, au hata kugombezwa kwa kilichotokea. Aidha, watoa huduma nchini Tanzania, kama ilivyo nchi nyingine, hawapatikani kwa wakati au hawana ujuzi na vifaa vya kutoa huduma ya ukatili wa kijinsia.Wasichana na wavulana wa Kitanzania waliulizwa (1) walimwambia mtu yoyote kuhusu yaliyowafika (2) walimwambia nani, kama kuna mtu waliyemwambia (3) waliomba msaada kwa ajili ya athari ya ukatili; (4) walipata msaada gani; na (5) kuna msaada gani zaidi walioutaka.

Watoto wengi hawatoi taarifa ya ukatili wa kijinsia. Takriban nusu ya wasichana na theluthi mbili ya wavulana waliokumbwa na ukatili wa kijinsia hawakutoa taarifa ya tukio hilo (angalia Mchoro 15). Zaidi ya asilimia 60 ya wasichana walitoa sababu za kifamilia au kijamii kwa kutokutoa taarifa, wakati asilimia 26 nyingine walitoa sababu binafsi. Zaidi ya theluthi ya waliotoa sababu za kifamilia/kijamii walisema hofu ya kutelekezwa au kutengwa ilikuwa sababu ya msingi ya kutotoa taarifa ya ukatili wa kijinsia. Miongoni mwa wasichana, sababu binafsi za kutokutoa taarifa za unyanyaswaji ni pamoja na: kutokuona ni tatizo, kuamini ilikuwa haimuhusu mtu mwingine au kuamini waliweza kukabiliana na tatizo hilo mwenyewe.

Kwa wavulana, walio wengi (asilimia 58) walitaja sababu binafsi za kutokumuambia mtu, ni pamoja na: kuamini haikuwa tatizo (asilimia 28). Wavulana wengine walisema waliamini haikumhusu mtu mwingine au kuamini waliweza kukabiliana na tatizo wenyewe. Asilimia thelathini na sita ya wavulana walitaja sababu za kifamilia au kijamii, pamoja na kutotaka kuiaibisha familia, kuogopa kutelekezwa au kuachwa, au kuogopa watu wasingewaamini. Miongoni mwa wasichana waliotoa taarifa, waliwaambia mama au baba zao (asilimia 41), au rafiki (asilimia 36), wakati wavulana waliwaambia zaidi marafiki (asilimia 71).

Mchoro 15: Sababu za kutomwambia mtu yoyote tukio la ukatili wa kijinsia lilitokea utotoni. Taarifa za waathirika wa ukatili wa kijinsia wenye miaka 13 hadi 24 ambao hawakumweleza mtu yoyote. (RUDWT 2009)[a]



[a]Asilimia ni kubwa kuliko 100 kwa sababu wasaili walitoa sababu nyingi za kutomwambia mtu yoyote tukio lao la kwanza la ukatili wa kijinsia.

Watoto wachache hutafuta huduma na wachache zaidi hupata huduma. Kwa ujumla takriban msichana 1 kati ya 5 na wavulana 1 kati ya 10 walitafuta huduma baada ya yaliyowasibu, lakini si wote waliotafuta huduma walipata. Takriban

msichana 1 kati ya 8 na mvulana 1 kati ya 20 walipata huduma kwa ajili ya yaliyowasibu katika ukatili wa kijinsia (angalia Mchoro 16). Wasichana waliopata huduma wanasema walipewa ushauri nasaha, huduma za kliniki au hospitali au msaada kutoka kwa mzee/ kiongozi wa jamii. Kati ya wavulana 9 waliopata huduma na kutoa taarifa 7 walitaja kupata ushauri nasaha.

Walipoulizwa kuhusu huduma zaidi, takriban asilimia 16 ya wasichana na wavulana walisema wangelipenda kupata huduma zaidi. Takriban nusu ya wasichana walitaka ushauri nasaha wakati asilimia 28 walitaka msaada wa polisi au afisa wa ustawi wa jamii. Asilimia 68 ya wavulana walitaka ushauri nasaha na 8 kati ya 37 walitaka msaada wa polisi au afisa wa ustawi wa jamii. Huko Zanzibar, idadi ya watoto waliotafuta huduma baada ya yaliyowasibu ilifanana, takriban 1 kati ya 5 ya wasichana na zaidi kidogo ya mvulana 1 kati ya 10. Isitoshe si wote waliosaka msaada walipata; zaidi kidogo ya nusu ya wasichana na wavulana walifanikiwa kupata huduma.

Mchoro 16: Waathirika wa ukatili wa kijinsia waliomwambia mtu, waliotafuta huduma na waliopata huduma. Taarifa za wavulana na wasichana wenye miaka 13 hadi (RUDWT 2009)



Ukatili utotoni na afya za Watanzania

Ukatili wa kijinsia unahusishwa na afya isiyoridhisha kwa wanawake. Wasichana wa Kitanzania wanaweza kuathirika sana kiafya kutokana na ukatili wa kijinsia utotoni. Kwa mfano, walipoulizwa kuhusu uzoefu wao katika siku 30 zilizopita, wasichana wa Kitanzania ambao waliwahi kukumbwa na ukatili wa kijinsia walikuwa na uwezekano mkubwa zaidi kuliko wasichana ambao hawakuwahi kushambuliwa:

- Kuwa na msongo wa mawazo (asilimia 59 kulinganisha na 41)
- Kuwa na hofu na kiwewe (asilimia 45 kulinganisha na 30)
- Kutoa taarifa ya kupimwa na kubainika na maambukizo ya ugonjwa wa zinaa (asilimia 8 kulinganisha na 4)
- Kunywa pombe (asilimia 10 kulinganisha na 3)

Wasichana wenye umri kati ya 13 na 17 waliotoa taarifa kuwa na ujauzito, wasichana 7 kati ya 49 walisema kuwa walau ujauzito mmoja ulisababishwa na kujamiiana kwa kulazimishwa au kushurtishwa. Miongoni mwa wenye miaka kati ya 18 na 24 waliotoa taarifa kuwa na mimba katika umri wowote, asilimia 6.3 walitoa taarifa kuwa walau ujauzito mmoja ulisababishwa na kujamiiana kwa kulazimishwa au kushurtishwa.

Ukatili ya kimwili pia unahusishwa na afya mbaya zaidi kwa wanawake. Wasichana waliowahi kukumbwa na ukatili wa kimwili walikuwa na uwezekano mkubwa zaidi kuliko ambao hawakuwahi kukumbwa na ukatili wa kimwili utotoni:

- Kuwa na afya ya wastani tu au mbaya (asilimia 25 kulinganisha na 15)
- Kuwa na hofu na kiwewe (asilimia 37 kulinganisha na 27)
- Kuwa na mawazo ya kujiua (asilimia 10 kulinganisha na 4)

Kwa wavulana wa Kitanzania hakukuwa na matokeo yoyote muhimu yaliohusishwa na ukatili wa kijinsia au kimwili utotoni. Isipokuwa Zanzibar, ambako wavulana waathirika wa ukatili wa kijinsia na/au kimwili walikuwa na uwezekano mkubwa zaidi kuwa wavutaji sigara, kuwa na msongo wa mawazo au hofu au kuwa katika afya mbaya.

Ukatili ya kiakili unaathiri afya kwa muda mrefu. Mwisho, watanzania wavulana kwa wasichana waliowahi kukumbwa na ukatili wa kiakili walitoa taarifa ya athari mbaya kiafya. Kwa mfano, wavulana waathirika wa ukatili wa kiakili utotoni walikuwa na uwezekano mkubwa zaidi kuliko ambao hawakuwahi kuwa waathirika wa:

- Kuwa katika hali ya wastani au mbaya kiafya (asilimia 35 kulinganisha na 23)
- Kujisikia unyonge (asilimia 61 kulinganisha na 46)
- Kuwa na hofu na kiwewe (asilimia 55 kulinganisha na 39)
- Kuwa na mawazo ya kujiua (asilimia 12 kulinganisha na 3)
- Kunywa pombe (asilimia 13 kulinganisha na 6)

Vivyo hivyo, wasichana wa Kitanzania waliokumbwa na ukatili wa kiakili walikuwa na uwezekano mkubwa zaidi kuliko ambao hawakuwahi kuwa waathirika wa:

- Kuwa na afya mbaya (asilimia 30 kulinganisha na 21)
- Kujisikia unyonge (asilimia 57 kulinganisha na 43)
- Kuwa na hofu na kiwewe (asilimia 45 kulinganisha na 31)
- Kuwa na mawazo ya kujiua (asilimia 16 kulinganisha na 6)

Kwa pamoja, athari hizi za afya za muda mfupi zinatia wasiwasi hasa kwa akina mama na wasichana. Kupunguza kuenea kwa ukatili dhidi ya watoto Tanzania kunaweza kupunguza matukio na gharama za matatizo ya afya ya akili na kimwili katika jamii.

Ukatili utotoni na tabia hatarishi

Utafiti mwingine unaonyesha kwamba waathirika wa ukatili wa kijinsia utotoni mara nyingi huwa na tabia hatarishi kingono katika ujana na utu uzima, kama vile kushiriki ngono kwa ajili ya malipo, kuwa na washirika wengi wa ngono, kuwa na washirika wa ngono wasio wa kutegemewa au kushiriki ngono na watu bila kupanga au kutegemewa, kutumia dawa za kulevya na pombe kabla au wakati wa kutenda ngono, na matumizi ya nadra ya kondomu au kutozitumia kabisa. Tabia zote hizi zinaongeza uwezekano wa kupata VVU na matokeo mengine hasi ya kiafya kama yalivyokwisha kuelezwa. Ushahidi wa Ripoti ya Ukatili Dhidi ya Watoto Tanzania (RUDWT) unaashiria kwamba kadhia za athari hizi za tabia hatarishi zinazosababishwa na ukatili wa kijinsia utotoni huenda pia zipo Tanzania.

Ukatili wa kijinsia unahusishwa na tabia hatarishi. Nchini Tanzania, matumizi ya nadra au kutokutumia kabisa kondomu katika miezi 12 iliyopita ni tabia ilioenea zaidi miongoni mwa wavulana na wasichana, walio na miaka kati ya 19 na 24, wenye historia ya kukumbwa na ukatili wa kijinsia utotoni kuliko wale wasio na historia hiyo. Kwa mfano, asilimia 46 ya wasichana waathirika walisema hawatumii kondomu wanapojamiiana ukilinganisha na asilimia 24 ya wasichana ambao si waathirika; asilimia 57 ya waathirika wavulana wa Kitanzania hawatumii kondomu wanapojamiiana ukilinganisha na asilimia 30 ya wavulana ambao si waathirika (angalia Mchoro 17).

Mchoro 17: Wasiotumia au waliotumia kondomu kwa nadra katika kipindi cha miezi 12 iliyopita ambao waliwahi kutendewa ukatili wa kijinsia utotoni. Taarifa za vijana wenye miaka 19 hadi 24 waliowahi kujamiiana. (RUDWT 2009)



[a]Ili kutambulika kama usiotumia kondom mara kwa mara au hutumii kabisa, wenye miaka 19 hadi 24 walitakiwa kutoa taarifa kama walijamiiana katika miezi 12 iliyopita - waliokwenye ndoa walitakiwa kutoa taarifa kama walijamiiana na washirika 2 au zaidi - na kama hawakutumia au walitumia kwa nadra kondomu wakati wa kujamiiana katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.

Wasichana na wavulana wa Kitanzania wenye historia ya kukumbwa na ukatili wa kijinsia utotoni walijamiiana zaidi na washirika wasiopungua wawili kuliko wale ambao hawakuwahi kukumbwa na ukatili. Kwa mfano, wasichana kwa wavulana ambao waliokumbwa na ukatili wa kijinsia utotoni walikuwa na uwezekano wa takriban mara dufu wa kufanya ngono na washirika wengi katika miezi 12 iliyopita kuliko wale wasio na historia ya ukatili huo (angalia Mchoro 18).

Mchoro 18: Washirika wengi wa ngono katika miezi 12 iliyopita wa waathirika wa ukatili wa kijinsia utotoni. Taarifa za wenye miaka 19 hadi 24 waliowahi kujamiiana. (RUDWT 2009)



Ukatili utotoni na Upimaji wa VVU

Ushahidi unaongezeka wa uhusiano kati ya ukatili, na hasa ukatili wa kijinsia, na VVU/UKIMWI na kuna maeneo makuu manne ya mwingiliano:

- Kujamiiana kwa nguvu au kwa kushurtishwa kunaweza kukasababisha maambukizi ya VVU.
- Ukatili au vitisho vya ukatili kunapunguza uwezo wa mtu kujadiliana mwafaka wa ngono salama.
- Kukumbwa na ukatili wa kijinsia utotoni kunaweza kusababisha tabia hatarishi katika maisha ya baadae (kama ilivyoelezwa hapo juu)
- Mtu anayekuwa muwazi kuhusu kuambukizwa kwake anaweza kuwa hatarini zaidi kukumbwa na ukatili kutoka kwa mshirika wake, familia au jamii.

Ukatili wa kijinsia hauathiri tabia ya kupima VVU. Kukumbwa na ukatili wa kijinsia utotoni na kujua vituo vya kupimia VVU havihusiani: wavulana na wasichana wa Kitanzania waliokumbwa na ukatili wa kijinsia utotoni walijua sehemu za kwenda kupima VVU kama vile ambao hawajawahi kuwa waathirika. Takriban wasichana 7 kati ya 10 na mvulana 1 kati ya 2 wenye miaka kati ya 13 na 17, ambao waliwahi kujamiiana walisema walijua wapi pa kwenda kupima VVU.

Vivyo hivyo, matukio ya ukatili wa kijinsia utotoni havikuhusiana na kiwango cha upimaji wa VVU. Miongoni mwa wasichana ambao walikuwa wamekwisha kujamiiana kabla ya kufikia miaka 18, asilimia 62 ambao waliokumbwa na ukatili wa kijinsia utotoni walitoa taarifa ya kupima VVU, ukilinganisha na asilimia 68 ambao hawakuwa wamekumbwa na ukatili wa kijinsia utotoni. Hakukuwa na tofauti kubwa katika asilimia ya wavulana waliotoa taarifa ya kupima VVU- asilimia 42 kwa wale ambao waliowahi kukumbwa na ukatili wa kijinsia utotoni ukilinganisha na asilimia 34 ambao hawakuwahi kukumbwa. Kazi zaidi lazima ifanyike ya kuvitambua na kuviondoa vizuizi vya kutaka kupima VVU kwa watoto wote, walioshambuliwa na wasioshambuliwa, kwa maana kasi ya upimaji bado ni ndogo.

5. Mitazamo kuhusu ukatili na unyanyaswaji Tanzania



Picha: UNICEF/Shehzad Noorani

5. Mitazamo kuhusu ukatili na unyanyaswaji Tanzania

DONDOO KUU

- Takriban asilimia 60 ya wasichana na zaidi ya nusu ya wavulana wenye miaka kati ya 13 na 24 walikubaliana kuwa ni sawa mume kumpiga mkewe katika mazingira fulani.
- Kwa wanawake wenye miaka kati ya 13 na 24, kuwa muathirika wa ukatili wa kimwili utotoni mikononi mwa ndugu kulihusishwa na kukubaliana na mume kumshambulia kimwili mke wake katika jambo moja au zaidi.
- Asilimia 5.2 ya wasichana wenye miaka kati ya 13 na 17 walitoa taarifa kufanyiwa tohara na asilimia 9.6 ya wanawake vijana wenye umri kati ya 18 na 24 walifanyiwa tohara.
- Asilimia 84 ya wanawake wa Kitanzania na asilimia 79 ya wanaume wa Kitanzania wanaamini tohara ya wanawake isitishwe katika jamii zenye mila hiyo.

Kanuni za jamii na utamaduni zinajenga jinsi wanajamii wanavyofikiri na kutenda. Mara nyingi hukumbatia maadili na taratibu za jamii na huashiria tabia zinazokubalika na zisizokubalika. RUDWT imeainisha kanuni nyingi za jamii na utamaduni zinazohalalisha ukatili Tanzania.

Unyanyasaji mke/mume

Wavulana na wasichana wa Tanzania katika utafiti waliulizwa kuhusu mitazamo yao kuhusu ukatili ya kimwili katika ndoa. Hususan, waliulizwa kama ilikubalika kwa mume kumpiga mke wake kama akitoka bila kuaga, hawajali watoto, anabishana nae, anakataa kujamiiana nae au anaunguza chakula.

Takriban nusu waliridhia ukatili wa kimwili kwa mke/mume. Takriban nusu ya wavulana (asilimia 52) waliamini ni sawa mume kumpiga mke wake katika walau jambo mojawapo, vilevile asilimia kubwa zaidi kidogo ya wasichana (asilimia 58) ilikubaliana na ukatili wa aina hii. Hususan wasichana ambao ni waathirika wa ukatili utotoni mikononi mwa ndugu walikuwa tayari zaidi kuunga mkono upigaji kuliko wale ambao hawakuwahi kuwa waathirika wa ukatili utotoni (angalia Mchoro 19). Hii inaashiria utamaduni wa ukatili wa kimwili unarithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Mchoro 19: Wanaounga mkono mume kumpiga mkewe kwa sababu moja au zaidi, kwa wale waliowahi kutendewa ukatili wa kimwili na ndugu utotoni. Taarifa za wenye miaka 13 hadi 24 (RUDWT 2009)



Unyanyaswaji wa watoto kijinsia

Unyanyaswaji wa watoto kijinsia, kama vile ukahaba wa watoto, ponografia ya watoto, na uuzaji na kufanya biashara ya kusafirisha watoto kunaweza kuwa na madhara makubwa kimwili, kiakili na kijamii ikiwa ni pamoja na kujeruhiwa na kupata ulemavu, ujauzito wa utotoni, matatizo ya ujauzito na vifo vya wanaojifungua, kudumaa kwa uwezo wa kuelewa, na magonjwa ya zinaa pamoja na VVU/UKIMWI. Ili kuelewa kuenea kwa unyanyaswaji wa watoto kijinsia Tanzania, wasichana na wavulana waliulizwa kama wamewahi kupokea pesa au zawadi/bidhaa ili wafanye ngono.

Viwango vya unyanyaswaji ni vidogo lakini kuna mwingiliano na waathirika wa ukatili. Asilimia nne ya wasichana wa Kitanzania wamewahi kupokea pesa au bidhaa ili wafanye ngono walau mara moja maishani mwao, na hasa wale waathirika wa aina tatu za ukatili. Asilimia themanini na mbili ya waliotoa taarifa ya kupokea pesa au bidhaa kufanya ngono pia walitoa taarifa ya ukatili wa kijinsia utotoni, asilimia 90 waliopokea pesa au bidhaa kufanya ngono walitoa taarifa walitendewa ukatili wa kimwili na ndugu, na asilimia 50 waliopokea pesa au bidhaa kufanya ngono walitoa taarifa ya kukumbwa na ukatili wa kiakili utotoni. Wavulana wachache wa Kitanzania walitoa taarifa ya kupokea pesa au bidhaa kufanya ngono.

Ukeketaji/tohara ya wanawake

Wasaili wengi wanaunga mkono kupigwa marufuku ukeketaji. Wasichana wa Kitanzania waliulizwa kama wamekeketwa. Takriban asilimia 5 ya wasichana wenye kati ya miaka 13 na 17, ukilinganisha na asilimia 10 ya wenye miaka kati ya 18 na 24 walisema wamekeketwa. Kwa sababu kosa hili linaadhibika kisheria, wasichana huenda wanasita kulitolea taarifa; hata hivyo, takwimu zinaendana na ripoti ya kuenea kwa ukeketaji iliyomo kwenye Utafiti wa Idadi ya Watu na Afya Tanzania 2010. Kwa kiasi kikubwa wasichana na wavulana wa Kitanzania wenye umri kati ya miaka 13 na 17 (asilimia 84 na 79, mtawalia) walisema desturi hiyo ikomeshwe.

Kwa pamoja matokeo haya yanaashiria kwamba kuna kanuni nyingi na maadili mengi yenye mizizi miongoni mwa Watanzania vijana ambayo ndiyo msingi wa kuunga mkono ukatili, haswa unaowalenga wanawake, ingawa kuunga mkono ukomeshwaji wa ukeketaji kunatia moyo. Ni muhimu kulikabili suala la kuhalalisha ukatili kijamii na kitamaduni nchini Tanzania ili mafanikio yatakayoleta mabadiliko yapatikane.

6. Tanzania itafanya nini kukabili tatizo la ukatili dhidi ya watoto?

Picha: UNICEF/Julie Pudlowski

6. Tanzania itafanya nini kukabili tatizo la ukatili dhidi ya watoto?

Changamoto kubwa ya kuboresha na kuimarisha sheria, afya na huduma za ustawi wa jamii nchini Tanzania ina sura mbili: kwanza, kuzishinda shinikizo za kijamii zinazowazuia watoto kutoa taarifa ya yaliyowasibu wanapofikwa na ukatili wa kijinsia, na pili, kuhakikisha kwamba watoto wakitafuta huduma, huduma zipatikane na zitolewe kwa upole na kwa kiwango bora. Pamoja na hayo, cha muhimu pia ni ufikishwaji taarifa kwa watu ambao watoto wana imani nao kama watetezi wao-wazazi na marafiki. Maelekezo kwenye huduma stahili lazima yaanze karibu na mahali ambako kwa kawaida ukatili unatokea-majumbani na shuleni-na mchakato ushirikishe watu wazima wanaoaminika pamoja na vijana.

Muingiliano mkubwa uliopo baina ya ukatili wa kijinsia, kimwili, na kiakili kama ilivyoainishwa hapo juu, aghalabu ukatili aina zote tatu ukimtokea mtoto mmoja, unaongeza ugumu wa tatizo. Matukio yote ya ukatili (kijinsia, kimwili, kiakili) lazima yatajwe, hasa pale ambapo tathmini hatarishi, mikakati na mipango inapofanywa ya kulikabili na kulizuia tatizo. Kwa mfano, kufunya kazi sambamba katika kuratibu na kushirikiana kunahitajika katika vyombo vyote vinavyohusika na ukatili ya kila aina.Vivyo hivyo kunahitajika uratibu na ushirikiano kati ya mifumo mbalimabli ya afya na ulinzi wa watoto, kwa mfano hospitali na kliniki, mipango ya ustawi wa jamii, na huduma za polisi na sheria. Matokeo yanaonyesha shule nyingi za Tanzania si salama, na mengi yanahitajika kufanyika kuhakikisha uratibu na ushirikiano katika sekta ya elimu unahakikisha usalama na ustawi wa watoto shuleni, katika jamii na wanapokwenda na kutoka shule.

Chini ya uongozi na maelekezo ya Kikosi Kazi Kinachojumuisha Sekta Mbalimbali (KKKSM), wizara za serikali, idara na wakala katika sekta za afya ya jamii, ustawi wa jamii, elimu, na sheria pamoja na asasi za kiraia zinaungana kutoa jibu la kuaminika na endelevu ndani ya Mfumo wa Kulinda Watoto wa Kitaifa.

Jibu halitapatikana mara moja, lakini kuna mengi yanayoweza kufanyika katika kipindi cha muda mfupi, wa kati, na mrefu kukabiliana, kuzuia na kutatua tatizo katika kila sekta muhimu. KKKSM kinapendekeza mbinu na mkakati utakaolenga kufanya yafuatayo:

Hatua za sasa

- Maafisa waandamizi wa serikali na wadau wafahamishwe kuhusu matokeo ya Utafiti kama sehemu ya maandalizi ya uzinduzi wa ripoti ya utafiti utakaohusisha viongozi wakubwa

- Uhamasishaji wa mwitikio wa sekta ya kiraia kushamirisha huduma zinazoongozwa na serikali za kulinda, kutetea na kuhamasisha.

- Kubuni na kuanza kutekeleza mkakati wa mawasiliano ili kujenga uelewa wa masuala yaliyoainishwa katika ripoti, hususan masuala ya kanuni za kitamaduni na kijamii yanayohalalisha ukatili na kuandaa mazingira ya mfumo wa utoaji taarifa, rufaa na kukabiliana kwa madhubuti zaidi na kupambana na unyanyaswaji na ukatili dhidi ya watoto.

- Kuendelea kusaidia wizara zinazoongoza Tanzania Bara (Wizara ya Maendeleo ya Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto) na Zanzibar (Wizara ya Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake, na Maendeleo ya Watoto) ili kuratibu kuzuia na kukabili ukatili dhidi ya watoto. Ikiratibiwa na KKKSM, mkakati huu wa sekta mbalimabli utagusa mifumo ya ustawi wa jamii, polisi na sheria; sekta za elimu, ustawi wa jamii, na afya; na mashirika na vikundi yanayojishughulisha na masuala ya VVU/UKIMWI, ukatili wa kijinsia, na maeneo mengine katika ngazi za kitaifa, kimkoa na kimtaa.

- Kufuatia matokeo ya utafiti, kuoanisha huduma zinazopatikana sasa za kuhudumia watoto waathirika wa ukatili, pamoja na kutathmini uwezo wa kutoa huduma za ushauri nasaha na sehemu za usalama kwa watoto na kupanga kipaumbele maeneo ya kusaidiwa.

Hatua za muda wa kati

- Kutunga taratibu na kanuni za kutekeleza Sheria ya Mtoto Na 21 2009 na kujenga mfumo wa mwenendo utakaofafanua na kugawa kazi na majukumu kisekta katika kuzuia na kukabili unyanyaswaji na ukatili dhidi ya watoto. Huko Zanzibar, kufanya kazi na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Maendeleo ya Watoto kutunga kanuni na taratibu za kutekeleza Muswada wa Watoto Zanzibar.

- Kuunganisha mipango na juhudi za kukabiliana na ukatili dhidi ya watoto ili uwe mfumo wa jamii unaofanya kazi, na kipaumbele cha kwanza kikiwa kumlinda mtoto wa Tanzania, kupitia mfumo wa Mpango wa Taifa wa Kazi Ulioanisha Gharama ya Mpango wa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi Zaidi (2011-2015), unaoratibiwa na Idara ya Ustawi wa Jamii.

- Kubuni "Mpango wa Kazi wa Taifa wa Kuzuia na Kukabili Ukatili Dhidi ya Watoto," utakaoimarisha Mpango wa Kazi wa Sekta wa Serikali ya Tanzania uliopo sasa, kwa kuweka miongozo na taratibu za uendeshaji kwa kila sekta, kutoka katika kanuni na taratibu zinazoandaliwa za Sheria ya Mtoto na Muswada wa Mtoto Zanzibar. Hii itajumuisha sekta zifuatazo, bila kubagua zinginezo:

    – Ustawi wa Jamii: Kubuni mfumo wa kufanya tathmini hatarishi ambazo zitaunganishwa na mfumo wa rufaa unaojumuisha sekta na huduma mbalimbali kubaini na kukidhi mahitaji ya ulinzi ya watoto ya muda mfupi na mrefu.

    – Shule: Kujumuisha ujumbe wa kuzuia ukatili wa kijinsia na sehemu salama kwenye programu za shule kuzungumzia jinsia, afya ya uzazi, na maendeleo ya jamii. Kuhakikisha elimu imeunganishwa katika mfumo wa rufaa wa sekta nyingi na mfumo wa kulinda watoto pindi haja inapojitokeza.

    – Polisi na Sheria: Kuimarisha na kupanua ulinzi stahili wa kisheria wa watoto na adhabu za kisheria kwa wakosaji; kuendeleza jitihada zilizopo kwenye Dawati la Jinsia na Watoto la Jeshi la Polisi kitaifa. Kuendelea kutoa elimu kwa polisi na maafisa wengine wanaohusika na usalama wa raia kuhusu ukatili dhidi ya watoto. Kubuni utaratibu wa pamoja wa uchunguzi na ustawi wa jamii, sekta ya afya na mamlaka na sekta zingine zinazohusika.

    – Afya: Kufanya kazi katika mfumo wa sekta nyingi kuhakikisha kuna miongozo iliyo wazi, dhahiri na rahisi kwa ajili ya matibabu, uangalizi, ufutiliaji na uzuiaji wa ukatili dhidi ya watoto. Kujenga jukwaa la wazi na stahili kwa ajili ya kujumuisha huduma rafiki na zenye tija kwa watoto ndani ya mifumo iliyopo ya kukabiliana na ukatili wa kijinsia.

- Kutambulisha na kuanzisha mikakati yenye vigezo na vipimo ya kuzuia na kukabili ukatili dhidi ya watoto ndani ya jamii, pamoja na kuanzisha na kutathmini gharama za mifumo ya ulinzi wa watoto katika wilaya zilizochanguliwa kwa ajili ya majaribio nchini Tanzania.

- Kubuni na kutekeleza kampeni ya kuhabarisha umma inayowalenga watoto wakubwa na vijana ili kuwafungulia njia za kutoa taarifa na inayoonyesha mikakati ya kuwasaidia watoto na vijana kupata habari na huduma.

- Kufanya utafiti kuhusu maoni na uzoefu wa watoto na watu wazima katika mahusianio ya shari na amani na kuyajumuisha haya kwenye programu ya uhabarishaji jamii ili kupambana na matumizi ya ukatili.

- Kusaidia mashirika yanayoshughulika na ustawi wa watoto ili kutokomeza ukatili dhidi ya watoto. Kuhakikisha kwamba watoto wenyewe wanashirikishwa katika kufuatilia na kutolea taarifa tabia na desturi zenye madhara kwenye jamii zao pamoja na kupinga uungwaji mkono tabia ya ukatili.

- Kuelimisha wazazi na watu wazima kuhusu tatizo na athari ya ukatili kwa watoto, pamoja na njia za kuwalinda watoto dhidi ya ukatili na jinsi ya kutambua dalili za unyanyasaji kama umekwishatokea. Ikibidi kuhimiza njia mbadala za kuadhibu bila ukatili.

- Kujenga na kutekeleza mfumo wa kusimamia na kutathmini, utakaopitiwa na KKKSM, kupima ushahidi kutoka wilaya teule juu ya mifumo ya kulinda watoto inavyoweza kupambana na ukatili dhidi ya watoto na kuweka mkakati wa kuusambaza mfumo nchi nzima.

Hatua za Muda Mrefu

- Kutegemea matokeo ya utekelezaji mwaka wa kwanza, kuandaa mfumo wa kusimamia na kutathmini inayogawa takwimu kwa njia tatu miongoni mwa sekta za ustawi wa jamii, elimu, polisi, sheria na afya ili kuwe na mfumo wa uchunguzi unaoshirikisha sekta nyingi katika kufuatilia mwenedo wa muda mrefu wa tatizo hili.

- Kujumuisha viashiria muhimu na maswali kutoka RUDWT, pamoja na ulinzi wa wasailiwa stahili unaozingatia maadili, kwenye tafiti za kitaifa zinazoendelea ili kuimarisha msisitizo wa ulinzi wa watoto katika tafiti za mara kwa mara za kitaifa.

- Kuendelea kuchanganua takwimu za utafiti ili kubaini mifumo inayoweza kusaidia mikakati ya uzuiaji na sera za umma, pamoja na kuoanisha hali hatarishi na yote yanayosaidia ulinzi ili kuelekeza jitihada za kuepusha madhara. Jitihada hii ishamirishwe na utafiti stahilifu ambao utawezesha uelewa wa kina zaidi wa muktadha wa ukatili na hatua zitakazostahili kuchukuliwa.

- Kufanya utafiti zaidi kuhusu ukatili dhidi ya vikundi vya watoto ambavyo havikufanyiwa utafiti na RUDWT 2009, kwa mfano watoto wa mitaani au wanaokaa kwenye nyumba za yatima.

- Kusaidia serikali ya Tanzania kuandaa mkakati wa ustawi wa jamii wa kuongeza rasilimali watu na uwezo wa Maafisa wa Ustawi wa Jamii kupambana na unyanyaswaji na ukatili dhidi ya watoto, kufuatana na dhima walio nayo chini ya Sheria ya Mtoto Na 21 2009, ili waweze kuwa waratibu na wasimamizi wazuri wa matukio katika mfumo wa taifa wa ulinzi wa watoto.

- Kutumia uzoefu na uwezo uliojengwa Tanzania kuhabarisha nchi nyingine za Afrika-Kusini mwa jangwa la Sahara kuhusu tatizo la ukatili wa watoto na njia zinazozingatia utamaduni zilizotumika kukabiliana nalo.

Mapendekezo haya lazima yaangaliwe katika muktadha wa utamaduni wa Tanzania na shughuli na mipango mingine iliyopo tayari inayolenga kuzuia na kupambana na ukatili dhidi ya watoto. Matokeo na mapendekezo yaliyomo katika ripoti hii yanatoa fursa kubwa ya kujenga mkakati wa kulinda watoto dhidi ya ukatili na hivyo basi kujenga mustakabali salama zaidi kwa ajili ya watu wa Tanzania.